Arusha, Tanzania

Tovuti: www.african-court.org

Simu: +255-272-510-510

AfCHPR
African Court on Human and Peoples' Rights

**MUHTASARI WA HUKUMU**

**CHACHA JEREMIAH NA WENGINE**

**DHIDI YA**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**MAOMBI YALIYOUNGANISHWA NA. 039/2019, 040/2019 NA 041/2019**

**HUKUMU KUHUSU UZINGATIAJI WA SHERIA NA FIDIA**

**5 JUNI 2026**

**UAMUZI WA MAHAKAMA YA AFRIKA YA HAKI ZA BINADAMU NA WATU**

**Arusha, 5 Juni 2026:** Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu (Mahakama) leo imetoa Hukumu katika kesi ya *Chacha Jeremiah na Wengine dhidi ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania*.

*Chacha Jeremiah, Methew Jeremiah Daud na Paschal Ligoye Mashiku* (Waleta Maombi) ni raia wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (Mjibu Maombi). Wakati wa kuwasilisha Maombi haya, walikuwa wamefungwa katika Gereza Kuu la Butimba, Mwanza, baada ya kukutwa na hatia ya mauaji na kuhukumiwa kifo, kwa kunyongwa. Waleta Maombi walidai kwamba Mjibu Maombi alikiuka haki yao ya kuishi, haki ya utu wa asili, haki ya kuwakilishwa na wakili wamtakaye, haki ya kuhukumiwa ndani ya muda unaofaa na haki ya kusikilizwa, zinazolindwa kwa mujibu wa Vifungu vya 4, 5, 7(1)(c), 7(1)(d) na 7(1) vya Mkataba wa Afrika wa Haki za Binadamu na Watu (Mkataba) mtawalia kuhusiana na kesi katika mahakama za kitaifa.

Kwa mujibu wa Kifungu cha 3 cha Itifaki ya Mkataba wa Afrika wa Haki za Binadamu na Watu kuhusu kuanzishwa kwa Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu ("Itifaki"), kwanza Mahakama iliangalia endapo ilikuwa na mamlaka ya kusikiliza Maombi hayo. Katika suala hili, Mjibu Maombi aliibua pingamizi kuhusu mamlaka halisi ya Mahakama akidai kwamba haina mamlaka ya kuwa mahakama ya rufaa.

Mahakama katika uamuzi wake, ilikataa pingamizi hilo, ikiona kwamba ilikuwa na mamlaka halisi kwa sababu Waleta Maombi walikuwa wamedai kuna ukiukaji wa haki zao, wakilindwa kwa mujibu wa Vifungu vya 4, 5, 7(1)(c), 7(1)(d) na 7(1) vya Mkataba.

Ingawa vipengele vingine vya mamlaka yake havikupingwa na Mjibu Maombi, Mahakama ilivichunguza kwa mujibu wa Kanuni zake. Katika suala hili, Mahakama ilibaini kuwa ilikuwa na mamlaka binafsi kwani, tarehe 29 Machi 2010, Mjibu Maombi iliweka Azimio kwa mujibu wa Kifungu cha 34(6) cha Itifaki. Azimio hili linaruhusu watu binafsi kuwasilisha maombi dhidi ya Mjibu Maombi kulingana na Kifungu cha 5(3) cha Itifaki. Mahakama ilisisitiza kwamba Mjibu Maombi kuondoa Azimio lake mnamo tarehe 21 Novemba 2019 hakukuathiri Maombi haya Yaliyounganishwa kwani uondoaji huo ulianza kutekelezwa mnamo tarehe 22 Novemba 2020, wakati Maombi haya yaliwasilishwa Mahakamani mnamo tarehe 21 Agosti 2019.

Aidha, Mahakama iliona kwamba ilikuwa na mamlaka ya muda kwa kuwa ukiukaji unaodaiwa ulitokea baada ya Mjibu Maombi kuwa mhusika wa Itifaki. Mwisho, ilibaini kuwa ilikuwa na mamlaka ya kieneo, ikizingatiwa kuwa ukweli wa jambo hilo ulitokea ndani ya eneo la Mleta Maombi.

Kisha Mahakama iliamua enapo Maombi haya yalikuwa yanakubalika kama ilivyoelezwa chini ya Kifungu cha 6(2) cha Itifaki na Kifungu cha 56 cha Mkataba, Kifungu cha 56 kama kilivyotajwa tena katika Kanuni ya 50(2) ya Kanuni za Mahakama. Katika suala hili, Mjibu Maombi aliibua pingamizi kuhusu ukubalifu wa maombi kuhusiana na Waleta Maombi kutokamilisha taratibu za ndani. Katika uamuzi wake, Mahakama ilisema kwamba Waleta Maombi walikuwa wamekata rufaa kwenda Mahakama ya Rufaa dhidi ya uamuzi wa Mahakama Kuu uliokuwa umewaweka kwenye hatia ya mauaji, chombo cha mahakama ambacho ni cha juu zaidi katika nchi ya Mjibu Maombi. Mahakama ya Rufaa ilitoa uamuzi wake tarehe 4 Aprili 2019, ikitupilia mbali rufaa ya Waleta Maombi. Kwa hivyo, Waleta Maombi walikuwa awmekamilisha taratibu za ndani kwa kuzingatia Kanuni ya 50(2)(e) ya Kanuni za Mahakama.

Ingawa masharti mengine ya ukubalifu hayakupingwa na Mjibu Maombi, hata hivyo Mahakama ililazimika kuhakikisha kuwa yametimizwa. Katika suala hili, Mahakama iliona kwamba, Waleta Maombi walikuwa wametambuliwa kwa majina kwa kutimiza Kanuni ya 50(2)(a) ya Kanuni za Mahakama. Iliona pia kwamba madai ya Waleta Maombi yalilenga kulinda haki zao kulingana na Kifungu cha 3(h) kuhusu malengo ya Sheria ya Kikatiba ya Umoja wa Afrika, na hivyo Maombi haya yalitimiza Kanuni ya 50(2)(b) ya Kanuni za Mahakama. Aidha, Mahakama ilibaini kwamba lugha iliyotumika katika Maombi haya haikuwa ya dharau au ya matusi kwa Mjibu Maombi au taasisi zake katika kutimiza Kanuni ya 50(2)(c) ya Kanuni za Mahakama. Maombi haya pia hayakutokana tu na habari zilizosambazwa kupitia vyombo vya habari, katika kutimiza Kanuni ya 50(2)(d) ya Kanuni za Mahakama.

Aidha, Mahakama ilibainisha kuwa Maombi haya ambayo yaliwasilishwa miezi minne na siku tatu baada ya Mahakama ya Rufaa kutoa uamuzi wake kuhusu rufaa yao, tarehe 4 Aprili 2019, yaliwasilishwa ndani ya muda unaofaa kwa mujibu wa Kanuni ya 50(2)(f) ya Kanuni za Mahakama. Mahakama pia ilijiridhisha kwamba Maombi haya hayakuibua madai ambayo tayari yalisuluhishwa mbele ya mahakama nyingine ya kimataifa. Matokeo yake, Mahakama ilitangaza kuwa Maombi hayo yanakubalika.

Kuhusu uzingatiaji wa sheria wa kesi hiyo, Mahakama iliangalia iliangalia endapo Mjibu Maombi alikuwa amekiuka haki za Waleta Maombi kwa mujibu wa Vifungu vya 4, 5, 7(1) (c), 7 (1) (d) na 7(1) vya Mkataba, kwa mwenendo wake katika tathmini ya ushahidi na kuwahukumu kifo Waleta Maombi.

Waleta Maombi walidai kwamba kutolewa kwa adhabu ya lazima ya kifo kunapinga uamuzi wa mahakama kuzingatia mazingira ya mshtakiwa na kosa husika. Mahakama iliona kwamba huu ni ukiukaji, kwani unakataa mchakato unaostahili kwa kuondoa uwezo wa afisa wa mahakama kutumia busara hiyo. Ilibaini zaidi kwamba ubadilishaji wa adhabu uliofanywa kuwa kifungo cha maisha haukuponya ukiukaji huo, kwani Waleta Maombi walikuwa tayari wamehukumiwa adhabu ya kifo ya lazima na

walikuwa wameshatumia muda wake kwenye jela ya waliohukumiwa kifo kabla ya kubadilishiwa adhabu.

Waleta Maombi walidai kwamba waliteswa wakati wakihojiwa wakiwalazimisha wakiri kosa. Mahakama iliona katika uamuzi wake kwamba Waleta Maombi hawakuwa wamewasilisha madai haya mbele ya Mahakama Kuu na kwamba hakukuwa na chochote kwenye kumbukumbu kuhusiana na kukiri huko ambacho kilihitaji mahakama za kitaifa ziingilie kati. Mahakama ilibaini kwamba Mjibu Maombi hakuwa amekiuka uhuru wa Waleta Maombi dhidi ya mateso kwa mujibu wa Kifungu cha 5 cha Mkataba.

Waleta Maombi pia walidai kuwa kutolewa kwa hukumu ya kifo kwa kunyongwa ni ukiukaji wa haki yao ya utu wa asili. Mahakama iliona kwamba njia ya kuuawa kwa kunyongwa ni kudhalilisha utu wa binadamu na kwa hivyo ni ukiukaji.

Kuhusiana na madai ya ukiukaji wa haki ya Waleta Maombi ya kuwakilishwa na wakili anayefaa, Mahakama iliona kwamba Waleta Maombi walipewa uwakilishi wa kisheria bila malipo na haikupata ushahidi wowote kwamba Mjibu Maombi alizuia Waleta Maombi wasipate wakili, kuzuia wasipate mashauri, au kuwanyima muda na nyenzo za kutosha kwa ajili ya maandalizi ya utetezi. Kwa hivyo, Mahakama iliona kwamba haki ya Waleta Maombi ya kuwakilishwa na wakili anayefaa waliyemchagua haikuwa imekiukwa.

Kuhusu madai ya ukiukaji wa haki ya kushtakiwa ndani ya wakati unaofaa, Mahakama iliona kwamba kipindi cha miaka mitano, miezi mitatu, na siku 15 kabla ya kuanza kwa kesi haukuwa muda usiofaa. Ilizingatia ugumu wa kesi hiyo, ikiwa ni pamoja na idadi ya mashahidi na uchambuzi wa ushahidi wa DNA, vilevile uhalisia wa muda mwingi kutumika katika michakato ya kabla ya kuanza kesi na mzigo wa kazi wa kitaasisi na upangaji ratiba.

Waleta Maombi walidai kasoro za kiutaratibu kuwa ni ukiukaji wa haki yao ya kusikilizwa kwa haki. Mahakama iliona kwamba haiwezi kuchukua jukumu la mahakama za ndani kwa kuchunguza tena utondoti wa ushahidi unaotumiwa kuthibitisha makosa ya jinai. Baada ya kupitia kumbukumbu hiyo, iligundua kuwa tathmini ya mahakama za kitaifa kuhusu ushahidi haikuonyesha kutofuata viwango husika vya haki za binadamu, kwa hivyo, hakuna ukiukaji uliobainishwa.

Kuhusu fidia ya kifedha, Mahakama ilitupilia mbali madai ya uharibifu wa mali ikisema kwamba Waleta Maombi hawakuwa wameonyesha uhusiano kati ya uharibifu wa mali na ukiukaji uliobainishwa. Hata hivyo, kwa kutumia busara zake kwa usawa, ilimpa kila Mleta Maombi, Shilingi za Tanzania Laki Moja (TZS 100,000) kwa sababu ya hasara ya kimaadili inayotokana na ukiukaji uliothibitishwa.

Kuhusu fidia isiyo ya kifedha, Mahakama ilitupilia mbali maombi ya Waleta Maombi ya kuachiwa huru, kwa kushindwa kuonyesha mazingira ya kipekee ya kulazimisha uamuzi huo kutolewa.

Mahakama, baada ya kubaini ukiukaji wa Vifungu vya 4 na 5 vya Mkataba, iliamuru Mjibu Maombi achukue hatua zote muhimu, bila kuchelewa, kuondoa kwenye sheria zake utoaji wa hukumu ya lazima ya kifo na kunyongwa kama njia ya kutekeleza hukumu ya kifo. Pia, Mahakama iliamuru Mjibu Maombi abatilishe hukumu hiyo, awaondoe Waleta Maombi kwenye adhabu ya kifo na asikilize tena kesi yao kuhusu hukumu kupitia utaratibu ambao unaruhusu busara ya mahakama. Aidha, Mahakama iliamuru Mjibu Maombi achapishe hukumu kwenye tovuti za Mahakama, na Wizara ya Katiba na Sheria ndani ya kipindi cha miezi mitatu tangu tarehe ya kupokea taarifa na kuhakikisha kuwa inapatikana kwa mwaka mmoja.

Kila upande uliamriwa kubeba gharama zake.

Kwa mujibu wa Kifungu cha 28(7) cha Itifaki na Kanuni ya 70 ya Kanuni za Mahakama, Jaji Rafaâ BEN Achour alitoa Maoni ya Kupinga kuhusu kugundulika kwa madai ya

ukiukaji wa haki ya kuhukumiwa ndani ya wakati unaofaa; Jaji Modibo Sacko alitoa Maoni ya Kupinga kwa Sehemu juu ya kiasi kilichotolewa kama fidia ya hasara ya kimaadili kwa Waleta Maombi; Jaji Dennis D. Adjei alitoa Maoni Tofauti kuhusu kugundulika kwa madai ya haki ya kuhukumiwa ndani ya muda unaofaa, athari ya kisheria ya kubadilishwa kwa hukumu ya kifo na kupewa kifungo cha maisha na aina ya fidia ambazo zinaweza kutolewa kutokana na hasara ya kimaadili; na Jaji Blaise Tchikaya na Jaji Dumisa B. Ntsebeza alitoa Maazimio kuhusu suala la adhabu ya kifo.

**Maelezo zaidi**

Maelezo zaidi kuhusu kesi hii, ikiwa ni pamoja na hati kamili ya uamuzi wa Mahakama ya Afrika, yanaweza kupatikana kwenye tovuti kupitia:
https://www.african-court.org/cpmt/details-case/0392019;
https://www.african-court.org/cpmt/details-case/0402019;
https://www.african-court.org/cpmt/details-case/0412019

Kwa maswali mengine yoyote, tafadhali wasiliana na Msajili kwa barua pepe kupitia registrar@african-court.org.

*Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu ni mahakama ya bara zima iliyoanzishwa na nchi wanachama wa Umoja wa Afrika ili kuhakikisha haki za binadamu na watu barani Afrika zinalindwa. Mamlaka ya Kisheria ya Mahakama kuhusu kesi na mizozo yote iliyowasilishwa kwake kuhusu tafsiri na utekelezaji wa Mkataba wa Afrika wa Haki za Binadamu na Watu na chombo kingine chochote cha Haki za Binadamu kilichoidhinishwa na Nchi zinazohusika. Kwa maelezo zaidi, tafadhali tembelea tovuti yetu www.african-court.org.*